# Muda wa katikati

## Tafakari ya Mwaka Mpya ya Jenerali Lyndon Buckingham

Wakati wa kuandika tafakari hii fupi nafurahia siku zilizo katikati ya Krismasi na Mwaka Mpya. Ni wakati wa likizo na mwendo ni wa pole zaidi kuliko kawaida. Naangalia nje juu ya milima mizuri, milima ya kijani na ni kimya na pana amani. Naweza kusikia akili na mwili wangu vikisema, 'aaaaahhhh'. Asante , Bwana, kwa siku za mapumziko na mrejesho.

Ni wakati sahihi wa kutafakari. Namshukuru Mungu kwa neema yake, huruma na upendo katika maisha yangu na maisha ya familia yangu. Natambua uaminifu wake kwa ahadi zake zote. Naweza kuona mkono wake katika kila tukio la mwaka 2023. Natambua bila kusita, mguso wa neema yake wa kuendeleza wakati wa mwaka uliojaa changamoto na uwezekano. Mungu ni mwema. Natafakari kuhusu nguvu ya maombi, uhai wa Neno la Mungu na furaha ya kushirikiana na watu wake. Natambua nafasi ya upendeleo ya kuhusika katika huduma ya Mungu kama ilivyodhihirishwa katika huduma ya utumishi wangu katika Jeshi la Wokovu Vile vile natoa shukurani kwa mguso wa huduma ya Jeshi la Wokovu duniani kote. Nawashukuru waumini wa Jeshi la Wokovu duniani ambao wametumika kwa uaminifu katika mwaka 2023, wengi wakifanya katika mazingira magumu sana. Uaminifu na kujitoa kwenu ni mhamasisho kwangu. Nayo yaleta tofauti katika dunia yetu.

Muda 'wa katikati' hushawishi mawazo kuhusu Mwaka Mpya. Nafahamu kuna watu wengi wanaoingia katika mwaka wakiwa na kiwango fulani cha wasiwasi, hofu na kutokuwa na hakika. Dunia ina mahangaiko mengi wakati huu. Taarifa zetu za habari zimejaa ripoti zinazoongeza wasiwasi wetu na kusababisha tujiulize mwaka utatuletea nini sisi sote.

Nimekuwa nikitafakari juu ya Maandiko fulani yanayonitia moyo na kunihamasisha ninapojiandaa kuukumbatia mwaka wa 2024.

Sefania 3:17 : 'Bwana, Mungu wako, yu katikati yako shujaa awezaye kuokoa. Atakushangilia kwa furaha kuu, atatulia katika upendo wake. Atakufurahia kwa kuimba.'

Maombolezo 3:22-23:'Ni huruma za Bwana kwamba hatuangamii, kwa kuwa rehema zake hazikomi. Ni mpya kila siku asubuhi; Uaminifu wako ni mkuu.'

Isaya 41:10: 'Usiogope,kwa maana mimi ni pamoja nawe, usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako, nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu.'

Pamoja na ahadi zilizo na uwepo wake, wokovu, upendo, nguvu na uaminifu, niko tayari kukumbatia changamoto na nafasi zinazoletwa na mwaka mpya. Je wewe?

Ingawa dunia inaweza kuwa imejaa kutokuwa na uhakika, huduma yetu duniani kama Jeshi la Wokovu inabakia kuwa yenye uhakika. Hebu tuendelee kuwa watu wanaompenda Mungu kwa kiwango cha juu, kila wakati tukitafuta nafasi za kumpa yeye utukufu na sifa kwa jinsi alivyo na kile alichotutendea katika Yesu. Hebu kila mara tuwe tayari kutoa sababu ya tumaini lililo ndani yetu. Twahitaji dunia ya Jeshi ilipuke na watu walio tayari kutangaza ile tofauti ambayo Yesu ameileta katika maisha yetu, kwamba kuokoka kunawezekana kwa yeyote kupitia kwa kumuamini yeye.

Nahitaji sisi tuendelee kuonyesha upendo wetu kwa Mungu kwa kuwapenda wengine, hasa wasiopendwa, walio katika mazingira hatarishi na wale wanaotengwa katika jamii. Kutafuta njia za kuwajali wengine huwa dhihirisho la matendo la thamani ya Ufalme wa Mungu.

Nahimiza wote sisi tudhamirie kabisa katika safari yetu ya uanafunzi katika mwaka 2024, kufuatilia utakatifu kila eneo la maisha yetu. Tafadhali tusichukulie kwa viwango vya chini nguvu na ushawishi ambao maisha matakatifu yanaweza kufanya kwa wale wanaotuzunguka. Maisha aliyoishi mtu kwa utukufu wa Mungu na hamu halisi ya kuwa manukato ya Kristo duniani yatakuwa na mguso. Mchango wetu binafsi unaweza kuwa mdogo, bali mkusanyiko wa mguso unaweza, na utakuwa muhimu.

Dunia inahitaji mchango tunaoweza kuutoa. Tunaweza kuwa wachache kwa idadi, lakini tunaweza na tutakuwa nguvu kubwa kwa mema tunapokuwa tuko wazi kuhusu huduma yetu, tukiwezeshwa na Roho Mtakatifu na tukiwa tayari kuhusika. Hesabu nimo ndani!

Neema na amani.

Mungu akubariki.

**Lyndon Buckingham**
Jenerali